

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA NANE

12 MEI, 2016



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA NANE – TAREHE 12 MEI, 2016

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Taarifa ya Mwaka ya Tathmini ya Utendaji wa Mamlaka ya Udhubiti wa Ununuzi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha, 2014/2015 (*The Annual Performance Evaluation Report of the Public Procurement Regulatory Authority for the Financial Year 2014/2015*).

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

150. MHESHIMIWA MAIDA HAMAD ABDALLAH (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Baadhi ya miradi ya maji inayosimamiwa na Halmashauri imekuwa ikisuasua kutokana na uchache wa fedha pamoja na kuingia mikataba na wakandarasi wasiokuwa na uwezo wa kutosha na kusababisha miradi hiyo kutokamilika kwa wakati:-

Je, Serikali imejipanga vipi kumaliza tatizo la maji kwa Wananchi wa vijijini.

WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

151. MHESHIMIWA JOEL MWAKA MAKANYANGA (CHILONWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya kutoka Makao Makuu ya Wilaya ya Chamwino kuelekea Kaskazini ni ya vumbi na ina madaraja mawili makorofi yaliyoko kati ya Chilonwa na Uzali na

lingine kati ya Dabalo A na Dabalo B, daraja lililopo kati ya Chilonwa na Nzali limewahi kuua watu mwaka 2014 na mifugo mingi pia imekufa kwenye daraja hilo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuyajenga madaraja hayo mawili ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Chilonwa.

**152. MHESHIMIWA ALI SALIMU KHAMIS
(MWANAKWEREKWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:-

- (a) Je, Shirika la Ndege la Tanzania ni Shirika la pamoja kati ya Tanganyika na Zanzibar;
- (b) Kama ndio, je Zanzibar ina asilimia ngapi katika shirika la ATCL;
- (c) Je, ni lini ATCL italipa deni la kodi ya kutua (*landing fee*) kwa Mamlaka ya Ndege Zanzibar.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

153.MHESHIMIWA MWITA MWIKWABE WAITARA (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Kumekuwa na utaratibu mbovu wa Mawaziri wa Elimu kuingilia shughuli za Mtaala kwa kubadilisha Mitaala, mfumo wa madaraja na hata aina ya Mitihani hasa kuweka maswali ya kuchagua katika somo la Hisabati:-

Je, ni lini Serikali italeta marekebisho ya Sheria ya NECTA ili Bunge libadili Sheria ya Baraza Kifungu cha 30 ili kuondoa nguvu ya Waziri ya kutoa maelezo bila kuhoji na hata bila kushirikisha Wataalamu wa Elimu.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

154.MHESHIMIWA FAIDA MOHAMMED BAKAR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-


Je, Serikali ina mkakati gani wa kuanzisha Benki ya wafanyabiashara wakubwa na wadogo ili kuwawezesha Wafanyabiashara hao (Wajasiriamali) kupata huduma iliyo bora kupitia Benki yao.

III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,
WAZEE NA WATOTO:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa Mwaka wa Fedha, 2016/2017.

(Majadiliano yanaendelea)



**DODOMA
12 MEI, 2016**

**DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE**